BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA MAWASILIANO ARDHI NA NISHATI YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA BAJETI YA WIZARA YA MAJI , NISHATI NA MADINI KWA MWAKA 2022/2023

**Mheshimiwa Spika,** Naomba nichukue fursa hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, ambae ametujaalia kukutana tena leo katika chombo hiki muhimu cha uwakilishi wa wananchi ili kujadili mambo mbali mbali muhimu kwa manufaa ya wananchi wetu ikiwemo suala zima la bajeti. Vile vile nakushukuru wewe binafsi pamoja na wasaidizi wako, kwa busara na maelekezo yenu kwa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ili iweze kufanikisha kazi zake za kila siku kwa ufanisi mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia imamshukuru sana Mheshimiwa Waziri , Mheshimiwa Naibu Waziri na uongozi wa Wizara kwa ujumla pamoja na watendaji wa Wizara ya Nchi, Fedha na Mipango Idara ya Bajeti kwa mashirikiano yao wakati Kamati yangu ikijadili Bajeti ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** Pia naomba kwa heshima niwashukuru wajumbe wa Kamati yangu kwa michango yao yenye tija na yenye lengo la kuimarisha ufanisi wa utendaji waliyoitoa wakati wa kujadili makadirio ya bajeti ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa mwaka 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika,** naomba niwatambue wajumbe hao kwa kuwataja majina kama ifutavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Yahya Rashid Abdulla | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Bahati Khamis Kombo | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Hussein Ibrahim Makungu | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Mussa Foum Mussa | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Kombo Mwinyi Shehe | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** shughuli za Kamati yetu zinaratibiwa na Makatibu wawili, ambao ni

1. Ndg. Rahma Kombo Mgeni na
2. Ndg. Himid Haji Choko

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ilipangiwa kukusanya shilingi **206,572,002,927** ambapo hadi kufikia tarehe 31 machi, 2022 Wizara imeripoti kukusanya Shilingi **128,28,803,826** sawa na asilimia **62%** ya makisio hayo. Kamati inaipongeza Wizara kwa hatua hii nzuri na tunaamini kwamba Wizara hadi kufikia mwisho wa mwaka huu wa fedha itavuka lengo walilokadiriwa.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na Makusanyo hayo ya jumla ya Wizara, lakini tukisoma kiambatanisho **Namba 2** katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri kinachoonesha makusanyo ya Wizara kitaasisi, tunagundua kwamba Mamlaka ya Maji Zanzibar (**ZAWA)** haijafanya vizuri kwani ilipangiwa kukusanya shilingi 10,870,491,200 ambapo ilifanikiwa kukusanya shilingi 2,519,123,782,49 sawa na asilimia **23%** tu ya makadirio. Makusanyo hayo yanaonesha uhalisia kwamba, bado kuna mwamko mdogo wa wananchi kuchangia huduma ya maji pamoja na taasisi mbali mbali zikiwemo za serikali kushindwa kulipia huduma hiyo. Kamati inaihimiza ZAWA kuongeza juhudi ya kutoa taaluma na kuweka mikakati ya kuhakikikisha kwamba wananchi na taasisi mbali mbali kuhusiana na kuchangia na kulipia huduma ya Maji ili iweze kufanikisha zaidi majukumu yake. Sambamba na hilo, Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha kwamba wananchi wote wanapata huduma ya maji safi na salama, kwani wananchi hawana mashaka ya kuchangia na kulipia huduma hiyo iwapo itapatikana kwa uhakika na ubora unaohitajika.

PROGRAMU ZA WIZARA

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu inaunga mkono uamuzi wa Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa kuendelea na Programu zake tatu kwa Mwaka ujao wa fedha zenye azma ya kuimarisha huduma za maji safi na salama pamoja na kuimarisha huduma za Nishati na Madini. Vile vile kuimarisha mazingira ya Utendaji kazi kwa watumishi wake.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa taarifa kwa Baraza lako tukufu kwamba, pamoja na hatua ya Kamati kuafiki na kuridhia kupitisha bajeti ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini ili kazi

iendelee, lakini tunaendelea kuhimiza utendaji na kujituma zaidi katika Mamlaka ya Maji na Shirika la Umeme ili kupata ufanisi wa upatikanaji wa Huduma ya Maji safi pamoja na nishati ya umeme kwa wananchi kama ilivyo azma na kasi ya serikali ya Awamu ya Nane katika kuwahudumia wananchi.

PROGRAMU YA USIMAMIZI WA HUDUMA ZA MAJI

**Mheshimiwa Spika,**pamoja na Kamati kuthamini juhudi za Serikali kupitia ZAWA kwa kufanikiwa upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi wote kwa asilimia 55% na kuacha pengo la asilimia 45%, bado tatizo la Mivujo, uhaba wa uzalishaji na uchakavu wa miundombinu ya maji pamoja na hujuma kwa mtandao wa maji kunaathiri matarajio ya lengo kuu la Programu ya Usimamizi wa Huduma za Maji ambalo ni kufikia Usimamizi endelevu na Usambazaji toshelevu kwa mujibu wa mahitaji.

**Mheshimiwa Spika,** ZAWA kupitia Hotuba ya Mhe. Waziri imeripoti kwamba hadi kufikia Machi 31, 2022 imefakiniwa kuziba mivujo 1,681 sawa na asilimia 39% ya mivujo 4,320 kwa mwaka huu. Hatua hii imepunguza wastani wa asilimia 3% tu ya upotevu wa maji katika mabomba yaliyopata hitilafu kwa maeneo ya Unguja na Pemba. Takwimu hizi zinaonesha dhahiri upotevu mkubwa wa maji unaosababishwa na uchakavu wa miundombinu ya kusambazia maji safi na salama na kuchangia kwa kiasi kikubwa ukosefu wa huduma hiyo kwa wananchi pamoja na kuashiria kazi kubwa inayowakabili ZAWA katika kuhakikisha kwamba maji yanayozalishwa yanawafika wananchi badala ya kupotea njiani.

**Mheshimiwa Spika,**Kamati inaendelea kuishauri ZAWA kuingia katika mifumo ya

kidigitali itakaoweza kubaini hitilafu yeyote ya maji katika vianzio na mitandao yake ya maji pamoja na kuimarisha ukaguzi wa mitandao yake. Aidha tunaishauri ZAWA kubadilika na kununua vifaa nyenye viwango, ubora na madhubuti ikiwemo mabomba na pampu za kusukumia maji ili kuweza kupunguza matatizo ya uunguaji wa Pampu na upasukaji wa mabomba ambayo nayo yanachangia ukosefu wa huduma ya maji na kuleta uzia kila uchao.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu inawaomba wajumbe kukubaliana na ombi la Wizara la kuidhinisha jumla ya shilingi **106,703,257,000,000** katika mwaka ujao wa fedha kwa ajili ya Programu **PN0301** ya Usimamizi wa Huduma za Maji, fedha ambazo ni nyingi ukilinganisha na shilingi **84,677,321,000** walizoidhinishiwa mwaka huu wa fedha unaomalizika. Kamati inaamini kwamba fedha hizo zitatosheleza katika usimamizi wa Huduma za Maji na kupelekea kuimarika kwa huduma hii na kuongeza idadi ya wananchi wanaopata huduma ya maji safi na salama.

## PROGRAMU YA USIMAMIZI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MADINI

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la Umeme ni miongoni mwa taasisi zinazotekeleza Programu ya Usimamizi wa Huduma za Umeme na Nishati ambapo viashiria vya muda mrefu vya kufanikiwa kwa Programu hii ni kuongezeka kwa asilimia ya huduma zinazotolewa kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaunga mkono azma ya Serikali kupitia ZECO ya kuhakikisha wananchi wote wanaungiwa umeme na wanafaidika na huduma hiyo kwa ukamilifu wake. Mhe. Spika pamoja na kuongeza Idadi ya wateja wapya hadi kufikia

asilia 62 ya matarajio, kwa upande mwengine ZECO inakabiliwa na changamoto kadhaa zinazohitaji kufanyiwa kazi ikiwemo kukatika katika mara kwa mara kwa umeme pamoja na umeme mdogo, na usiokuwa na nguvu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha unaomalizika ZECO imepanga kubadilisha nguzo mbovu 1,620 badala yake hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2022 ZECO ikalazimika kubadilisha nguzo 1,859 sawa asilimia 115% na kuvuka malengo waliyojiwekea. Kadhalika katika kipindi hicho ZECO ilifanya ukaguzi maalum kwa transfoma zake na kubaini jumla ya transfoma 48 zilikuwa na hitilafu mbali mbali. Changamoto hizi zote bado zinaakisi umakini unaohitajika wakati wa kuaagiza vifaa vya miundombinu ya Umeme.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inadhani mpangilio wa miundombinu ya umeme pamoja na kutofanyiwa ***Service*** za mara kwa mara kwa miundombinu hiyo, pamoja na uchakavu wa waya, mita na nguzo nako kunachangia matatizo ya upatinaji wa huduma hiyo. Kamati kwa msisitizo mkubwa inaishauri ZECO nayo kuwa makini wakati wa kuagiza vifaa vilivyo bora kwa kuzingatia viwango na vigezo vinavyohitajika, ili vifaa hivyo viweze kudumu kwa muda mrefu na kuondosha dhana ilijengeka katika jamii kwamba miundombinu ya ZECO haina viwango.

**Mheshimiwa Spika,** mnamo mwezi Januari mwaka huu, Kamati yetu ilifanya kikao na Watendaji Wakuu wa TANESCCO, kikao ambacho pia kiliwashirikisha Watendaji wakuu wa Wizara ya Maji, Nishati na Madini ya Zanzibar pamoja na watendaji wa ZECO. Katika kikao hicho TANESCO ilielezea azma yake ya kutaka kuiuzia umeme ZECO kwa

**shilingi 130.0 kwa Unit Moja,** lakini kwa wakati huo bodi ya wakurugenzi ya ZECO ilikua bado haijakaa ili kujadili na kuidhinisha bei hiyo iliyopendekezwa na TANESCO.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inayo taarifa kwamba tayari Bodi ya ZECO imesharidhia bei hiyo mpya iliyopendekezwa lakini hadi Kamati inapitia Bajeti hii, suala hili lilikuwa limekwama kupata baraka za uongozi wa Wizara ya Maji, Nishati na Madini ya Zanzibar. Kamati inamuomba Mheshimiwa Waziri kuliingilia kati suala hili, ili hatimae liwasilishwe TANESCO ili nayo ianze kuiuzia Umeme ZECO kwa bei mpya ambayo italeta unafuu mkubwa kwa wananchi wa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu inazo taarifa kwamba Mradi wa uwekaji waya wa pili wa umeme kutoka Ubungo hadi Mtoni chini ya ufadhili wa Serikali ya Marekani kupitia Shirika la Changamoto za Millenium (MCC), ZECO ilikabidhiwa *Optic Fibre* yenye njia 24 iliyojumuishwa katika waya wa umeme kwa lengo la kupata fedha zitakazosaidia katika utunzaji wa miundombinu hiyo na matengenezo ya baadae yatakapojitokeza. Utafiti wa Kamati umebaini kwamba, sehemu kubwa ya *Fibre* hiyo inatumiwa na Kampuni ya ZANTEL pamoja na *E-Government.* Kamati yangu inaendelea kuwa na wasiwasi wa mapato yanayopatikana katika sehemu hii.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (ZURA), Kamati yangu inaunga mkono juhudi za ZURA kwa kutanua wigo hadi kufikia hatua ya kudhibiti sekta ndogo ya gesi kwa waingizaji na wasambazaji wa bidhaa ya gesi za majumbani. Aidha kamati ilifanya jitihada za kukutana na wafanyabiashara hao ambapo Kamati ilipata mshangao mkubwa sana baada ya

kulalamikiwa kwamba wanakabiliwa na tatizo la Kodi zipatazo 11 hadi kuifikisha Gesi hiyo kwa mwananchi. Kamati inaiomba Wizara na Mamlaka zinazohusika kulifuatilia suala hili linalopelekea gesi hiyo kupanda bei kila mara na mzigo huo kubebeshwa mwananchi wa kawaida. Tunaiomba Serikali idhibiti moja kwa moja bei ya gesi hiyo huku ikizingatia faida kwa wafanyabiashara unafuu kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** Tukigusia suala la rasilimali zisizorejesheka ambapo mheshimiwa Waziri katika Hutuba yake ameahidi kujipanga ili kuendelea kudhibiti utoroshwaji wa rasilimali hizo kwa kuweka mazingira bora ya utoaji wa huduma, hili ni jambo jema na Kamati tunaliunga mkono. Hata hivyo Udadisi wa Kamati umebaini kuwa katika kipindi cha Julai 2021 hadi Februari 2022 kuna kesi takriba 99 zinazohusu kuchimba, kusafirisha na kuuza mchanga bila ya kibali. Tunaiomba Serikali kutoa ufafanuzi wa suala la mchanga kwani limekuwa likileta utata na manunguniko kwa wananchi kuhusiana na upatikanaji wa nishati hii hivi sasa.

PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA MIPANGO YA WIZARA

**Mheshimiwa Spika,** Nimalizie hutuba yangu kwa kugusia Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Mipango ya Wizara. Mheshimiwa Spika, katika vipindi tofauti tumekuwa tukisikia hadithi za Mipango ya Wizara ya utayarishaji wa Mpango Mkuu Umeme wa Zanzibar, pamoja na Umeme mbadala, Kamati inaihamiza Wizara kuharakisha kukamilisha Mpango huu ili kubaini mahitaji halisi ya umeme pamoja na njia bora ya kupata nishati hiyo kwa uhakika na bei nafuu hapa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza hayo sasa napenda kukushukuru wewe binafsi

Mheshimiwa Spika pamoja na wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza kwa makini wakati nikitoa maoni ya Kamati ya Mawasilano, Ardhi na Nishati kuhusiana na Bajeti hii pamoja na kuwaomba wajumbe wa Baraza lako kuijadili kuichangia na hatimae kuipitisha kama walivyoomba.

**Mhe. Spika**, kwa niaba ya wajumbe wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati na a niaba ya Wananchi wa Jimbo la Kwahani naunga mkono hoja hii ya Makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maji,Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika**, Naomba kuwasilisha.

**Ahsante,**

**……………………………**

**(Mheshimiwa Yahya Rashid Abdulla MAMBA),**
**Mwenyekiti,**
**Kamati ya Mawasiliano,Ardhi na Nishati.**
**Baraza la Wawakilishi**
**Zanzibar.**